KWA JINA LA ALLAAH, MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

25/= Ksh

Volume 9, Issue 5

25th Jumâ al-Awwal 1432

29th April, 2011

YALIYOMO

KUMSHUKURU ALLAAH 1 - 4

TANGAZO LA DARSA 1

BIASHARA KWA MIKOPO 4

FADHLA ZA KUMSHUKURU ALLAAH

FIQH UL-AD'IYYAH WAL-ADHKAAR

Mtayarishi: Sheikh 'Abdur-Razzaaq Ibn 'Abdul-Muhsin al-'Abbaad al-Badr

Hapana shaka kuhusu fadhla kubwa za *Shukr* na daraja zake, kumshukuru Allah (سبحانه وتعالى) kwa baraka zake za kudumu, malipo yake yenye kuendelea na msaada wake usio na kifani. Allah ameamrisha kuwa na shukrani katika Kitabu chake na akaharamisha kinachopinga hiyo (shukrani). Naye vilevile amewasifu watu wa shukr na akawasifu kuwa wao ni watu makhsusi miongoni mwa viumbe vyake. Allah vilevile akatujuza yakwamba watu wa shukr hufaidika kutokamana na Aya Zake na Allah (سبحانه وتعالى) akaziorodhesha dalili za shukr na akaitilia hima. Allah (سبحانه وتعالى) akaamuru watu wawe ni wenye kushukuru katika zaidi ya sehemu moja kwenye Kitabu chake, akasema Allah: **"Na shukuruni ne'ma ya Mwenyezi Mungu ikiwa kweli mnamuabudu Yeye."**[an-Nahl (16):114]

Na akasema Allah (سبحانه وتعالى): **"Na nishukuruni, wala msinikufuru."** [Baqarah(2):152]

Na akasema Allah (سبحانه وتعالى): **"Takeni rizki kwa Allah na mwabuduni na mshkuruni. Kwake mtarudishwa (siku ya kiyama)."** [al-Ankaboot(29):17]

Allah akalinganisha shukr na *eemaan* na akaeleza yakwamba Yeye hana haja ya kuadhibu viumbe vyake ikiwa watakuwa na shukurani kwake na ikiwa ni wenye kumuamini Yeye. Allah (سبحانه وتعالى) amesema, **"Allaah hakuadhibuni kama mtashukuru na mtaamini. Na Allaah ndiye mwenye kupokea shukrani na ndiye Mwenye kujua."** [an-Nisaa (4):147]

Allah vivile ameeleza kuwa watu wa shukr ni wenye kustahiki baraka zake miongoni mwa waja wake, akasema: **"Na namna hii Tumewafanyia mtihani baadhi yao (viumbe, yaani matajiri) kwa baadhi (yao wengine walio makafiri) ili waseme (walio matajiri): "Jee, hao ndiwo Allaah Amewafanyia ihsani miongoni mwetu (pasina kutufanyia sisi? Uwongo huo, si dini ya haki hiyo kama wameijua wao kabla yetu." Basi Allah akasema). Je, Allah hawajui wanaomshukuru?** [al-An'aam (6):53]

Allah ameinasibisha nyongeza kwenye Shukr, kuwa ni nyongeza isiyokuwa na mwisho kama ambavyo Shukr haina mwisho wake, Allah akasema, "**Na kumbuka alipotangaza Mola wenu wallahi mkishukuru nitawazidishia, na wallahi mkikufuru adhabu yangu ni nzito**" [Ibraheem (14):7]

Kwahivyo shukr kwa Allah ni jambo la milele na kwa sababu hii imesemekana "kila ikiwa hujioni katika hali yakuongezekewa basi kuwa na shukurani"

Allah amewagawanya watu katika sampuli mbili: walio na shukrani (shukoor) na wasio na shukurani (kufoor) na linalo mchukiza Yeye zaidi ni kufr na watu wake, na

TANGAZO LA DARSA

MASJID MAZRUI *[KILA SIKU BA'DAL MAGHRIB]*

JUMATATU - JUMANNE / [*Bulugh ul-Maraam*] / Ustadh Athman Bin Na'man

JUMATANO - ALKHAMIS / [*Nawaaqidh ul-Islaam*] / Ustadh Athman Bin Na'man

IJUMAA - Tafseer ul-Qur'an [*Ustaadh Ismaa'il*]

JUMAMOSI / [*Arba'oon an-Nawawee*] / Abu 'Abdur-Razzaq Haruna Khamis

Unaweza kusikiliza Darsa hizi kwenye Mtandao (Internet)

Pal-talk ⟹ All-Rooms ⟹ Religion & Spirituality ⟹ Callers to Tawheed ⟹ Swahili Duroos

linalompedeza Yeye ni shukr na watu wake. Amesema Allah, "**Hapana shaka sisi tulimuekea mwanadamu njia ima ni mwenye kuamini au ni mwenye kukanusha.**" [Insaan (76):3]. Na amesema Allah, "**Mkikanusha, basi hapana shaka Allah hana haja nanyi, lakini haridhii kufuru kwa waja wake: na kama nkishukuru, hayo yanamridhisha kwenu.**" [Zumar (39):7].

Na amesema: "**Na wallahi hakika tulimpa Luqmaan fahamu (na tulimwambia) hapana shaka mshukuru Allah. Na atakaye mshukuru Allah hapana shaka thawabu za kumshukuru zitamfaa mwenyewe. Na atayekanusha hapana shaka Allah ni Mkwasi, Mwenye kuhimidiwa.**" [Luqmaan (31):12]

Na akasema Allah (سبحانه وتعالى): "**Na atakae shukuru hapana shaka manufaa yake yatamrudia mwenyewe. Na atakaye kufuru basi hapana shaka Mola wangu ni Mkwasi, Mkarimu.**" [an-Naml (27):40].

Allah aeleza kuwa wale wanaomshukuru ndiwo wanaomuabudu Yeye Peke yake na wale wasiomshukuru Yeye si watu wenye kumuabudu Yeye, kwani amesema (سبحانه وتعالى): hamuabudu kwani Allah asema, "**... na mshukuruni Allah ikiwa Yeye peke yake mwamuabudu.**" [Baqaraa (2):172]

Na akasema (سبحانه وتعالى): "**Na kama mkishukuru, hayo yanamridhisha kwenu.**" [Zumar (39):7]

Jambo la kwamza katika maarisho ya Allah ni shukr Kwake na wazazi wake mtu mwenyewe, "**Natumemuamrisha mwanadamu awafanyie wema wazazi wake wawili. Aliichukua mimba mamake kwa udhaifu juu ya udhaifu (siku baada ya siku mpaka kumzaa) na kumnyonyesha kwake ni baada ya kutimia miaka miwili. Na (tulimwambia) nishukuru mimi na wazazi wako wawili kwangu mimi ni marudio.**" [Luqmaan (31):14]

Allah anatoa mno katika njia ya malipo kwa vitendo vingi vya Ibada kulingana na Apendavyo Yeye, Amesema: "**Na mkichelea ufukara basi atawakwasisha Allah kutokana na vipawa vyake apendapo.**" [Tawbah (9):28]

Akasema Allah katika kujibu du'aa: "**... na awaondolee mnayomuomba na kusahau mnayomshirikisha nayo.** " [al-An'aam (6):41]

Allah asema kuhusu Rizk: "**humruzuku amtakaye.**" [Baqarah (2):212, Aali'-Imraan (3):37, Noor (24):38, Shoora (42):19].

Na kuhusu msamaha, Allah amesema: "**humsamehe amtakaye.**"[Aali'-Imraan (3):129, Maa'idah (5):18, Al-Fath (48):14]
Amesema Allah katika Surat at-Tawbah:"**Amsamehe Allah amtakaye.**" [Tawbah (9):15]

Ama kuhusu kuwa ni mwenye kushukuru (shukr), kuna thawabu aina kumi zenye kuhusiana nayo, kwani Allah amesema: "**Na tutawalipa wenye kushukuru**" [Aali -'Imraan (3):145]. Na akasema: "**Na Allah atawalipa wenye kushukuru.**" [Aali-Imraan (3):144]

Allah atueleza kuwa adui wa Allah, Iblees, anajitahidi kuwawekea wanaadamu kizuizi ili wasiwe na shukurani, kwa sababu alizingatia kuwa ni utukufu wa hali ya juu, daraja na cheo kikubwa. Iblees akasema, kama alivyosema Allah: "**Kisha Wallaahi nitawajia wao, nitawajia wao mbele yao, nyuma yao, upande wao wa kulia na upande wao wa kushoto. Na wala hutowapata wengi wao ni wenye kushukuru (wenye kukutwi'i).**" [al-A'raaf (7):17]

Vilevile Allah ametueleza kuwa wanaomshukuru Yeye ni watu wachache. Akasema Allah: "**Na ni wachache miongoni mwa waja wangu wenye kumshukuru Allah (kwa neema Zake)**" [Saba (34):13]

Na akasema Allah: "**Lakini wengi ya watu hawashukuru.**" [Baqara (2):243, Yoosuf (12):38, Ghaafir (40):61]

Allah ameeleza kuwa shukr ndio lengo la kumba na kutokamana na baraka Zake nyingi: "**Na Allah aliwatoa katika matumbo ya mamazenu hamjui kitu chochote. Na amewajaalia masikio na macho na nyoyo. Hapana shaka mtashukuru.**" [Nahl (16):78]

Na akasema Allah: "**Na miongoni mwa Rehma yake (ne'ma) amewaumbia usiku na mchana ili mupumzike ndani yake (usiku) na ili mzitafute fadhla zake (rizki - wakati wa mchana) na hakika mshukuru.**" [Qasas (28):73]

Na akasema, "**Na ni Yeye (Allah) aliyeidhalilisha bahari ili mule kutokana na bahari nyama safi (samaki) na mtoe humo pambo (johari, lulu na kadhaalika) mlivaalo. Na utayaona majahazi (vilevile Meli) yakata maji humo na ili mupate kunufaika kwa vipawa vyake na hapana shaka mutashukuru.**" [Nahl (16):14]

Ayah zilizo na maana hizi ni nyingi, na shukr vile vile ndio njia ya Mitume na Manabii wa Allah ambao ndio viumbe watukufu wa Allah na wale ambao wako karibu na Yeye (عليهم السلام). Allah amemsifu Mtume wake wa kwanza aliye Mtume kwa watu wa ardhi kwa sababu ya shukrani yake Allah akasema: "**Enyi kizazi cha wale tuliowachukua (jahazini) pamoja na Nuh, hapana shaka yeye alikuwa ni mja mwingi wa kumshukuru Allah.**" [al-Israa (17): 3].

Katika sifa za Nooh (عليه السلام) za kipekee hapa katika kutaja na kuwahutubia waja kuwa ni kizazi chake yaonyesha kuongozwa kwao kupitia yeye (Nooh) ni baba yao wapili baada ya Aadam. Hakika Allah hakuleta kizazi ila kupitia kizazi chake, Allah asema, "**Na tulikifanya kizazi chake wao ndio waliobakia.**" [Saaffaat (37):77]

Allah amewaamuru watoto wake Nooh

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

wajifananishe na baba yao katika kumshuku Allah, kwani kwa hakika alikuwa ni mja mwenye shukurani. Allah amemsifu rafiki Yake wa karibu Ibraheem (عليه السلام) kutokana na shukurani zake, Allah akasema: **"Hapana shaka Ibraahim alikuwa na Ummah wenye kumtwi'i Allah wenye kuziwacha dini zote zisizo za sawa na wala hakuwa ni miongoni mwa washirikina. Ni mwenye kuzishukuru neema zake (Allah). Alimchagua (Allah) na kumwongoza kwenye Uislamu."** [an -Nahl (16):120-121]

Allah alieleza kuwa Ibraheem (عليه السلام) alikuwa ni Ummah: ikimaanisha kuwa alikuwa ni kigezo bora na alikuwa mnyenyekevu mwenye kumtwi'i Allah. Kisha Allah akamsifu kwa sifa hizi kwa sababu alikuwa ni mwenye kushukuru neema za Allah (سبحانه وتعالى). Kwahiyo shukr ndilo lililokuwa lengo la rafikiye (عليه السلام). Allah alimuamrisha Moosa (عليه السلام) apokee aliyompa kutokana na ujumbe na kuzungumza nae kwa unyenyekevu. Allah akasema: "**Alisema (Allah) 'Ewe Musa, hapana shaka Mimi nimekuchagua kwa watu (wa zama zake) uwafikishie ujumbe wangu na maneno yangu, basi yashike niliyokupa ya utume na ilmu na uwe ni miongoni mwa wenye kushukuru."** [al-'A'raaf (7):144]

Ayah zenye kuchukua maana hii ni nyingi katika kuifahamisha shukurani ya Mitume (عليهم السلام) nakuwa hii ndiyo njia na muelekeo wao. Ama kuhusu shukrani ya Mtume wa mwisho, bwana wa kizazi cha Adam, Muhammad Ibn Abdillah (صلي الله عليه وسلم) - basi mlango ni mpana katika mas'ala haya na bahari ina kina kikubwa. Kwa hakika yeye ni maarufu mno kwa hilo mbele ya Allah (سبحانه وتعالى) ambaye ni mvumilivu aliyesimama wima katika kumnyenyekea Allah, aliye na shukurani zaidi kwa neema za Allah, na aliye na daraja ya juu zaidi kuliko wengine mbele ya Allah. Imesahihishwa katika swaheeh kutoka kwa al-Mugheerah bin Shu'bah (رضي الله عنه) kuwa alisema: Mtume (صلي الله عليه وسلم) alikuwa akisimama kuswali mpaka miguu yake ikifura, basi akaulizwa (صلي الله عليه وسلم). "Lakini si Allah ameshakusamehe madhambi yako yaliopita na yatakayotokea? Akajibu (صلي الله عليه وسلم): "Basi na mimi sifai kuwa ni mja mwenye kushukuru?" [al-Bukhari]

Malaika, Manabii, Mitume naWaumini wote wamtakia Rehma na Amani kama ambavyo Allah alivo...

KUHUSU UHAKIKA WA SHUKRANI NA MAHALI PAKE KWA SALAF

Mazungumzo yaliopita yalikuwa ni kuhusu fadhla za shukr na daraja yake kubwa mbele ya Allah na ushahidi uliotajwa katika Qur'an, sasa tutayazungumza misingi ya shukr na uhakika wake na marejeo kuhusu hali za Salafus-Saalih zilivyohusiana na daraja yake.

Ama kuhusu msingi wa shukr na hakika yake basi ni kule kukubali neema kutoka kwa mwenye kuneemesha pamoja na unyenyekevu na mahaba:

Yoyote asiyejua neema alizopewa ni mjinga nazo na hana shukurani na neema hizo. Na yoyote ajuae neema alizopewa lakini asimjue mwenye kuneemesha basi pia si mwenye kushukuru. Yoyote azijuae neema alizopewa na mwenye kuneemesha lakini akakataa neema, kama yule anayezikataa neema za mwenye kuneemesha amekufuru kwazo. Yoyote ajuae neema na akajmua mwenye kuneemesha na akazikubali neema bila kuzikataa lakini si mnyenyekevu kwa Mwenye kuneemesha wala hapendi wala haridhiki na Mwenye kuneemesha neema hizo basi naye hajawa mwenye kushuru kwa neema hizo alizoneemeshwa. Na yoyote ajuae neema na kumjua Mwenye kuneemesha neema hizo na akazikubali na kunyenyekea kwake, akawa na upendo na akaridhika na Mwenye kuneemesha na akatumia neema hizo kwa njia zenye kuonyesha mahaba yake na utiifu wake kwa Mwenye kuneemesha - huyo ndiye Mwenye shukrani kwa neema hizo. [Ibn ul -Qayyim, Tareeq ul-hijratayn, Uk.175]

Kwahivyo kwa haya ni wazi kuwa shukr ina misingi mitano: unyenyekevu wa mwenye kushukuru kwa yule mwenye kushukuriwa; mahaba ya mwenye kushukuriwa (yaani: Allah); kukiri kuwa Allah amekuneemesha; kumsifu na kumtukuza kwa kukuneemesha; kutotumia neema hizo katika njia anazozichukia Allah. Mambo matano haya ndiyo misingi mitano ya shukr, na yale yaliyojengewa juu ya shukr, kwa hivyo ikiwa mojawapo ya misingi hiyo hautapatikana, basi hukmu za shukr itakuwa zimetingishwa. Shukr ni kwa moyo, ulimi na viungo. Ni kwa moyo unapokuwa mnyenyekevu, Umakinifu na mahaba, ni kwa ulimi pindi unapomtaja Allah na kukubali neema zake, na ni kwa viungo pindi vinapofanya utwiifu. [Ibn ul-Qayyim, madaarij us-saalikeen, vol.2, Uk. 246]

Ibn Abee Dunyaa (رحمه الله) ameeleza kwenye kitabu chake *ash-Shukr* kuwa mtu alimwambia Abee Haazim Salamah ibn Deenaar (رحمه الله): "Ni nini shukr ya macho ewe Abaa Haazim?" Abu Hazim akasema: "Ni kwamba uonelee kwayo (hayo macho) yaliyo mazuri na utaje hayo na ukiona maovu kwayo uyafiche hayo." Kisha yule mtu akasema: "Ni nini shukr na masikio?" Aboo Hazim akasema "Ni kuwa usikie kwayo mazuri na uwe ni mwenye kutega sikio kwa hayo (mazuri) na ni kusikia maovu na uyapuuze hayo maovu." Kisha yule mtu akauliza: "Ni nini shukr ya mikono?" Akasema Aboo Hazim: "Ni kuwa haichukuwi kisicho haki yake na haizuwii haki za Allah." Kisha akauliza yule mtu " Ni nini shukr ya sehemu za siri?" akajibu kama asemavyo Allah (سبحانه وتعالى): "**Na ambao wao kwa tupu zao ni wenye kuzihifadhi. Isipokuwa kwa wake zao au vijakazi vyao. Hapana shaka wao si wenye**

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 3)

kulaumiwa. Basi yoyote atakaefanya kinyume ya haya basi wao hakika ndio wenye kuikiuka mipaka (ya Allah).” [al-Mu’minoon (23): *5-7*].

Ama kuhusu yule ambaye ana shukrani na ulimi wake lakini hana shukurani na viungo vyake vilivyobaki. Basi huyu ni mtu anayefanana na mtu mwenye koti lakini halivai na matokeo yake ni kwamba hafaidiki kutoka na mvuke, baridi, umande, na theluji. Neema ya Allah juu ya mja wake katika matamshi yake, mikono yake, miguu yake na mwili mzima haina mipaka na yote hayo huwajibisha unyenyekevu kwa Mwenye kuneemesha. ’AbdurRahmaan bin Zayd ibn Aslam **(**رحمه الله**)** amesema: Shukr huchukuwa nguvu za sifa, misingi yake na matawi yake, kwa njia hii mtu afaa aangalie neema za Allah kwenye mwili wake, masikio, macho, mikono, miguu na mengine yasiyokuwa hayo, kwani hakuna kingine katika hizo ila kwa baraka za Allah. Ni haki ya mja kutumia neema alizopewa na Allah kwenye kiwiliwili chake kwa njia ya kuwa mtiifu kwa Allah. Vilevile kuhusu neema nyingine kama riziki mja atakiwa afanye amali na neema hiyo kwa njia ya utwi’ifu kwa Allah. Kwa hiyo yoyote atakaefanya amali njema na neema hizo atakuwa anastahiki sifa kwa kuung’ata kwa mkono wake, msingi na matawi yake. .[Ibn Abee Dunyaa---ash-shukr,no.157]

Kutokamana na baraka za Allah juu ya mja wake ni yale ambayo Aliyompa katika afya njema kwenye masikio yake, kuona kwake na kiwiliwili kizima. Na vilevile ni kama ambavyo Allah alivyomneemesha mja kwa makao mazuri na Afya njema basi kwa yote hayo yatakiwa mja awe ni mwenye kunyenyekea na kushukuru.

Ununuzi kwa (njia ya) Mkopo kwa Bei ya Kuzidisha

Na: Sheikh al-Albaani **(**رحمه الله**)**

Suali: Ni nini hukmu ya kununua kitu kwa njia ya mkopo kwa bei ya kuzidisha (Installments)?

Jawabu: Kwanza kabisa, ununuzi wa njia ya mkopo kwa bei ya kuzidisha ni uzushi (bid'ah) wa vitendo ambavyo havikuwahi kuwepo wala kujulikana miongoni mwa Waislamu katika vizazi vilivyotutangulia. Bali hayo ni miongoni mwa jinsi walizoachiwa na makafiri, wale ambao, katika siku za nyuma, ndiwo waliowanyang'anya ardhi zao, wakawatawala na kuwaweka chini ya himaya yao na sheria zao za ukafiri. Kisha walipoamua kuhama kutoka kwenye miji hiyo mikuu, waliziwacha nyuma athari zao zilizo mbovu na zenye upotofu. Na leo, Waislamu wamekuwa wanaishi juu ya mila hizo na vitendo walivyoachiwa na makafiri.

Vilevile kuna jambo jengine - ambalo ni muhimu sana - nalo ni kama alivyosema Rasoolullaah **(**صلى الله عليه وسلم**)**: **"Sikuwaachia jambo lolote lenye kuwakurubisha kwa Allaah, isipokuwa niliwaamuru kuyatekeleza. Na Sikuwaachia jambo lolote lenye kuwatenga mbali na Allaah, na kuwakurubisha zaidi na Jahannam, isipokuwa nimewakataza kuyatekeleza."** [1]

Kutokana na haya, tunaona yakwamba Mtume Muhammad **(**صلى الله عليه وسلم**)** aliyakataza yale ambayo siku hizi yanajulikana kwa **"ununuzi kwa njia ya mkopo kwa bei ya kuzidisha (installments)."** Kwahivyo, shughuli hizi za kibiashara ni mambo ya uzushi, ambayo hayakuwa yakijulikana na Waislamu waliotutangulia. Pia nataka kusema yakwamba hili jina lenyewe (asli yake) ni jambo la uzushi kwani hayapatikani mas-ala hayo katika vitabu vya Fiqh kwa jina kama hilo "ununuzi kwa njia ya mkopo kwa bei ya kuzidisha (installments)." Bali, kwapayikana katika vitabu vya Kiislamu, mambo kama vile *Ad-Dain* (deni) na pia *Al-Qard-ul-Hasan* (deni zuri). Deni hili (la pili) ndilo limekuwa, katika maisha ya kila siku ya Muislamu, ni jina tu lisilofungamana na mipango maalum au makisio ya aina yoyote. Huko kote ni kuhimizwa katika kumpa mtu deni lililo zuri na zaidi ya hayo, ingawa kulingana na Mtume **(**صلى الله عليه وسلم**)**, ukopeshaji wa dollar mbili ni mkama uliyejitolea dollar moja kwa njia ya sadaqa. Hii ina maana:

Umkopeshapo ndugu yako Muislamu dollar mbili, ni kama uliyetoa sadaqa ya dollar moja mfukoni mwako. Kama ambavyo Mtume **(**صلى الله عليه وسلم**)** alivyohimiza kuhusiana na deni zuri kama hili, vilevile amekataza kuchukua pesa zaidi kutokana na kuchelewa kwa malipo ya ndugu yako ya mapatano hayo.

Mtume **(**صلى الله عليه وسلم**)** amesema: **"Yeyote mwenye kujitengezea aina mbili za biashara zinazotokamana na biashara moja, basi atapata emma kilicho kichache kati ya viwili au faida (riba)."** Na katika hadeeth nyengine, **"alikataza kufanya njia mbili za kibiashara kutokamana na (biashara) moja."** Msimulizi wa hadeeth hii aliulizwa kuhusu maana ya makatazo hayo, nae akajibu: "Maana yake ni kwamba pale usemapo: 'Nitakuuzia kitu hichi kwa kiasi kadhaa cha pesa taslimu, na kwa kiasi kadhaa (cha zaidi) pesa taslimu kwa malipo ya polepole."

Nitakuuzia chombo hichi kwa dollar 100 taslimu sasa hivi, na kwa dollar 105.00 kwa njia ya malipo ya polepole, yaani kama deni. Mtume **(**صلى الله عليه وسلم**)** akasema: **"Yeyote mwenye kujitengezea aina mbili za biashara zinazotokamana na biashara moja, basi atapata emma kilicho kichache kati ya viwili au faida (riba)."** Hii ina maana yakwamba iwapo atachukuwa pesa za ziada, basi hiyo inakuwa ni riba, kama ilivyo-onekana katika mfano wa chombo kilichouzwa kwa kiasi cha dollar 105, dollar tano zaidi kwa ajili ya ucheleweshaji.

Kama pangelikuwa na hukmu za ki-Sheria za Kiislamu kwa watu na viongozi, basi mnunuzi huyu aliyehadaiwa na kunyang'anywa dollar tano zaidi kama malipo ya mfanyi biashara akingojea ucheleweshaji wa malipo hayo, angelikuwa na haki ya kumkamata na kumshtaki kwa Wanavyuoni. Kwahivyo, huu ndiwo ufahamu wa hadeeth hii. Kitu chenye kuuzwa ni kimoja, Lakini uuzaji wenyewe unakuwa ni wa aina mbili za kibiashara: Pesa taslimu za kiwango kadhaa zenye kulipwa bila ya kukawia na kwa malipo ya polepole ya kiwango hicho. Kwahivyo uongezaji wa pesa kwa ajili ya kuchelewa kuzilipa kwa mara moja umebainishwa kuwa ni riba na Mtume **(**صلى الله عليه وسلم**)**.